# HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI (W)

## TAREHE 22/04/2022

***WAJUMBE WALIOHUDHURIA:***

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** | Mh. Amani J. Kasinya | - Diwani Kata ya Gombero | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mh. Kadiri R. Fuliza | - Diwani Kata ya Manza | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mh. Salehe N. Mtindi | - Diwani Kata ya Mkinga | Mjumbe |
| 4. | Mh. Bakari A. Mkusa | - Diwani Kata ya Bwiti | Mjumbe |
| 5. | Mh. Mwanakombo A. Gobeto | - Diwani Kata ya Daluni | Mjumbe |
| 6. | Mh. Mwanahawa S. Mashango | - Diwani Viti Maalum | Mjumbe |
| 7. | Bw. Edwin Mwampamba | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | **Katibu** |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA: KWA TAARIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** | Mh. Dunstan Kitandula | - Mbunge Jimbo la Mkinga | Mjumbe |

***WATAALAMU WALIOHUDHURIA:***

1. Bw. Amiri Mganga - Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
2. Bw. Mohamed Kombo - Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Shule
3. Bw. Ally Kisuda - Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
4. Bw. Octavian Moshiro - Mkuu wa Idara ya Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika
5. Bw. Moses A. Kibula - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
6. Bi. Suzana Ndegeleki - Kaimu Mkuu wa kitengo cha TEHAMA
7. Bw. Thomas J. Mnkande - Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu
8. Bw. Paul Ntandu - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
9. Eng. Castory Keneth - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
10. Bi. Hawa Hassan - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
11. Bw. Omari Mashaka - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
12. Bw. Husein Kitojo - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango
13. Bi. Susana Joseph - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
14. Bw. Masudi Salumu - Mkuu wa Kitengo cha Ugavi

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| KATIBU | MWENYEKITI |

15. Bi. Maria Dagobert - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
16. Bw. Shabani Maliwa - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
17. Bw. Hayuda Mpumi - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
18. Bw. Geofrey Julius - Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara

**Waandishi**

1. Bw. Ally Odongo
2. Bi. Mwajuma Mavura

**MUHT.NA.114/11/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwakaribisha Wajumbe kwenye kikao na alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao naye aliwakumbusha Wataalam juu ya umuhimu wa kikao hiki na umakini uwe ni wa lazima kwa kuzingatia maslahi mapana ya Wananchi wa Wilaya ya Mkinga na alifungua kikao rasmi saa 06:42 Mchana.

**MUHT.NA.115/11/2021/2022: KUPITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Katibu aliwasilisha agenda za kikao na Wajumbe walizipitisha kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kupitisha agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 24/01/2022 Bajeti, 24/01/2022 Hoja na 30/03/2022.
4. Utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 30/03/2022.
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Machi 2022.
6. Kuwasilisha majina ya nyongeza ya watia saini (Signatory) kwa akaunti ya Halmashauri Makao makuu.
7. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi kwa Kipindi cha Mwezi Julai 2021 Hadi Machi 2022 kwa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Fedha za Bakaa ya Mwaka wa Fedha 2020/2021.
8. Taarifa ya Ukaguzi kwa kipindi cha Robo ya Tatu Januari-Machi 2022.
9. Mapendekezo ya kufuta Hoja za miaka ya nyuma za mkaguzi wa nje kuanzia 2010/2011 hadi 2018/2019 kwa mujibu wa Waraka Na. 1 wa Waziri Mkuu wa mwaka 2015.

.................................... ....................................

**KATIBU** **MWENYEKITI**

10. Taarifa ya Mikopo ya Asilimia kumi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.
11. Taarifa ya kesi za Halmashauri zilizopo mahakamani kwa kipindi cha Robo ya Tatu Januari- Machi 2022.
12. Rasimu ya sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga za mwaka 2022.
13. Taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya tatu.
14. Taarifa ya manunuzi kwa Kipindi cha Robo ya Tatu Januari- Machi 2022
15. Ombi la mabadiliko ya matumizi ya fedha
16. Mengineyo.
17. Mashauri ya Nidhamu.
18. Kufunga kikao.

Baada ya kuwasilisha agenda hizo, Wajumbe walizipitisha na kuwa agenda sahihi za kikao hicho.

**MUHT.NA.116/11/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 24/01/2022 BAJETI, 24/01/2022 HOJA NA 30/03/2022.**

Katibu aliwasilisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 24/01/2022 Bajeti, 24/01/2022 Hoja na 30/03/2022. Baada ya kuwasilisha Wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa ili kufanya masahihisho ambapo hakukuwa na marekebisho na Muhtasari ulisainiwa na Katibu na Mwenyekiti na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**MUHT.NA.117/11/2021/2022: UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 30/03/2022.**

Azimio lilitekelezwa na kupatiwa ufumbuzi.

**MUHT.NA.118/11/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI MACHI 2022.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Mapato na Matumizi kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022** iliidhinishiwa bajeti ya Shilingi **23,197,474,223.** Katika kiasi hicho mapato ya ndani ni Shilingi **1,370,894,280.00,** ruzuku toka Serikali kuu kwa ajili ya

.................................... KATIBU

.................................... MWENYEKITI

mishahara ni Shilingi **13,589,331,433.00;** Shilingi **1,144,395,250.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Ruzuku ya Miradi ya maendeleo ni Shilingi **7,092,853,260.00**.

**MAPATO**

Mapato ya Halmashauri yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni mapato kutokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri, ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mishahara, Matumizi mengineyo na Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo.

**Mapato kutoka vyanzo vya ndani:** Kwa mwezi **Machi 2022**, Halmashauri imekusanya kiasi cha Shilingi **178,070,756.65** kutoka mapato ya ndani, kati ya fedha hizo mapato ya ndani yasiyolindwa ni Shilingi **168,611,502.65** na mapato lindwa (NHIF, Papo kwa hapo, CHF na Ada za Sekondari) ni Shilingi **9,459,254.00.** Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** Halmashauri imekusanya jumla ya Shilingi **1,286,794,986.14.** Mapato haya sawa 93.87**%** ya lengo la Mwaka.

**Mapato ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida:** Kwa mwezi **Machi 2022**, Halmashauri imepokea ruzuku yenye thamani ya Shilingi **1,300,936,975.6.** Kati ya fedha hizo Shilingi **1,055,869,559.00** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **245,067,416.65** kwa ajili ya mapato mengineyo.

Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** Halmashauri imepokea Jumla ya Shilingi **10,496,070,167.85,** kati ya fedha hizo mapokezi kwa ajili ya Mishahara ni Shilingi **9,735,158,918.00** na mapato mengineyo ni Shilingi **760,911,249.85.** Mapokezi haya sawa **71.2%** ya lengo la Mwaka.

**Mapato ya Miradi ya Maendeleo:** Kwa mwezi **Machi 2022** upande wa Miradi ya Maendeleo ya Fedha za Ruzuku Jumla ya kiasi cha Shilingi **603,433,052.30** kimepokelewa. Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** jumla ya kiasi cha Shilingi **5,508,141,164.14** kimepokelewa sawa na **77.6%** ya lengo la Mwaka. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na mapato ya ndani jumla ya Shilingi **59,315,573.00** zimepokelewa. Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** jumla ya kiasi cha Shilingi **317,482,449.98** kimepokelewa.

................................ KATIBU

................................ MWENYEKITI

MATUMIZI:

**Matumizi Maeneo yasiyo ya Ruzuku:** Kwa mwezi **Machi 2022** Matumizi yaliyofanyika ni Shilingi **88,419,311.65.** Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** jumla ya kiasi cha Shilingi **679,458,090.85** kimetumika sawa na **67.4%** ya lengo la Mwaka.

**Matumizi Maeneo ya Ruzuku:** Kwa mwezi **Machi 2022** Halmashauri imetumia kiasi cha Shilingi **1,087,591,159.00,** kati ya fedha hizo Mishahara ni Shilingi **1,054,812,059.00** na matumizi mengineyo ni Shilingi **32,779,100.00. K**uanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** jumla ya kiasi cha Shilingi **10,056,664,238.12** kimetumika ikiwa Shilingi **9,728,098,680.00** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 369,795,114.52,** kwa ajili ya matumizi mengineyo ambayo ni sawa na **68.2 %** ya lengo la Mwaka.

**Matumizi ya Miradi ya Maendeleo:** Kwa mwezi **Machi 2022** kiasi cha Shilingi **722,579,222.00** kimetumika katika Miradi ya Maendeleo ya fedha za ruzuku. Kuanzia mwezi **Julai 2021** hadi **Machi 2022** Jumla ya Shilingi **3,678,882,606.10** zimetumika sawa na **52%** ya lengo la Mwaka.

**Orodha ya wadaiwa wa Halmashauri.** Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga inadai jumla ya kiasi cha Shilingi **240,765,019.77** kutoka mfuko wa Wanawake, Vijana, Watu wenye ulemavu, Masurufu na Wadaiwa wa mapato ya ndani (Defaulters).

**Salio la fedha katika akaunti za Halmashauri hadi tarehe 31/03/2022 kama inavyoonekana katika jedwali:-**

| No | Jina la Akaunti | Namba | Kiasi (Cash) |
|---|---|---|---|
| 1. | Own Source (Mapato) | 42310000707 | 117,834,064.25 |
| 2. | General Fund (Malipo) | 9921210101 | 38,310,420.06 |
| 3. | Amana (Mapokezi) | 42310000704 | 62,565,819.44 |
| 4. | Amana (Malipo) | 9921169787 | 38,915,244.51 |
| 5. | Maendeleo | 9921210301 | 53,143,891.19 |
| 6. | Matumizi Mengineyo | 9921210901 | 251,022,137.00 |
| 7. | Elimu | 9921210501 | 109,579,032.34 |
| 8. | Afya | 9921210601 | 21,201,055.35 |
| 9. | Mishahara | 9921210801 | 11,812,438.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 0 | Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu (Mapokezi) | 43710000085 | 64,574,195.70 |
| 11 | Development special fund | 9921210301 | 18,224,111.73 |
| 12. | Development local | 9921180001 | 755,000,000.00 |
| | **JUMLA** | | **1,542,182,409.57** |

**MAJADILIANO**

Baada ya kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi yalifanyika majadiliano na Wajumbe walitoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

a) Mwenyekiti aliwapongeza Wataalam kwa kuwezesha kuongeza mapato hadi kufikia 93.87%na alisisitiza juhudi ziendelee kuimarika zaidi katika kusimamia suala zima la ukusanyaji wa mapato.

b) Mjumbe alitoa pongezi za dhati kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa mapato ya ndani na kusimamiwa vizuri na Halmashauri.

c) Mjumbe alitaka kupatiwa ufafanuzi wa kiasi cha shilingi 3,000,000/= kimetumika vipi kwa ajili ya umeme wa Jengo kwa mwezi Machi na Aprili,2022.

Katibu alijibu kuwa kiasi kilichotajwa kimetokana na matumizi mbalimbali ya umeme ndani ya Halmashauri, hata hivyo taarifa ya kiasi hicho kimetokana na uhalisia wa malipo taslimu (cash base) kwa matumizi ya umeme yaliyofanyika kwa miezi miwili.

**Iliazimiwa** kwamba Mkurugenzi awasiliane na Meneja Tanesco ili waweze kuangalia tatizo la gharama kubwa za umeme kwenye Jengo la Halmashauri.

d) Mjumbe alitaka kupata ufafanuzi kuhusu utaratibu uliotumika katika ununuzi wa magari mawili ya Halmashauri.

Katibu alijibu kuwa yaliwasilishwa maombi maalum kwenye bajeti na kiliombwa kibali Ofisi ya Waziri Mkuu. Majibu ya kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Hazina yamewapa jukumu GPSA la kuratibu mchakato wa manunuzi ya magari hayo.

e) Mjumbe alitaka kufahamu kuwa magari hayo yamepangiwa katika Idara gani. Katibu alijibu kuwa kwa sasa hayajapangiwa lakini atayapangia kazi katika Idara yoyote.

............................................ KATIBU

............................................ MWENYEKITI

**f)** Mjumbe alishauri kuwa katika msimu ujao chanzo cha ushuru wa karafuu kiangaliwe zaidi katika ukusanyaji wa mapato na aliomba tuongeze juhudi katika vyanzo vilivyobaki.

**g)** Mjumbe alieleza kuwa karafuu kwa sasa zinapakiwa kwenye gari na wafanyabiashara wanazificha chini ya viti vya magari na aliomba suala hili liangaliwe na wakusanyaji wa mapato wanatakiwa wachunguze katika magari ya abiria.

Aidha Mwenyekiti aliomba zoezi hili la ukaguzi lianzie katika Tarafa ya Maramba.

**Azimio** Afisa kilimo umwagiliaji na ushirika afuatilie suala la ukaguzi wa magari ya abiria ili kuyabaini yanayosafirisha karafuu.

Baada ya majadiliano hayo taarifa ilipitishwa na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

Katibu aliwasilisha taarifa ya kuomba kuongezwa kwa Watia saini kwa akaunti ya Halmashauri Makao Makuu kuwa Kundi “A” kwa sasa yapo mawili, yaani Zahara Abdul Msangi (Mkurugenzi ) na Jwani Maria Yengi (Mweka Hazina), hivyo kupendekeza kuongeza jina la Mhasibu Mmoja wa Matumizi Ndugu Geofrey Julius Mwambashi kuwa mtu wa tatu katika kundi hilo.

Vilevile kundi “B” linawatia saini watatu ambao ni Octavian Adam Moshiro, Joseph Ligoha na Omari Kombo Mtunguja. Ndugu Omari Kombo Mtunguja amepata uhamisho, nafasi yake ipo wazi. Hivyo kupendekeza jina la Ndugu Erasto Kalist Msigwa Mkuu wa kitengo cha Nyuki kuwa mtu wa tatu kutia saini kundi “B”.

Wajumbe kwa pamoja waliyapitisha mapendekezo hayo na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**MUHT.NA.120/11/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2021 HADI MACHI 2022 KWA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA FEDHA ZA BAKAA YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Miradi kwa Kipindi cha Mwezi Julai 2021 Hadi

....................... ......................
KATIBU MWENYEKITI

Machi 2022 kwa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Fedha za

Bakaa ya Mwaka wa Fedha **2020/2021,** ambapo alieleza kuwa katika mwaka wa fedha **2021/2022**, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilivuka na fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Shilingi **768,179,292.47.** Kiasi tajwa hakijumuishi fedha za Elimu bure na hadi kufikia tarehe **31/03/2022** jumla ya **Shilingi 600,965,630.76** zimeshatumika.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **6,003,819,600.00.** Jumla hii haijumuishi fedha za Elimu bure bali ni fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi **485,455,600.00** ni kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Hadi kufikia tarehe 31/03/2022, Halmashauri imepokea jumla ya Shilingi **2,537,515,376.63** sawa na asilimia **42.27** ya bajeti idhinishwa ya miradi ya maendeleo na imetumia kiasi cha Shilingi **1,539,395,992.28** sawa na asilimia **60.67** ya fedha zilizopokelewa.

**FEDHA NJE YA BAJETI**

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga imepokea fedha nje ya Bajeti kiasi cha Shilingi **2,308,051,794.23** kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha, kwa ajili ya kutekeleza mpango wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31/03/2022, jumla ya Shilingi **1,414,461,102.19** zimetumika sawa na asilimia **61.28** ya mapokezi ya fedha hizo.

**MAJADILIANO**

**a)** Mjumbe alishauri kuwe na mpangilio mzuri wa muda na idadi ya vikundi vinavyokopeshwa katika taarifa inayowasilishwa.

**b)** Mjumbe alitaka kufahamu kuhusu idadi ya mabati yaliyonunuliwa katika ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Zingibari.

Katibu alijibu kuwa atalifanyia kazi.

**Azimio** kikao kijacho iwasilishwe idadi ya Vifaa vya ujenzi (Mabati) yaliyonunuliwa katika shule ya Sekondari Zingibari.

**c)** Mjumbe alitaka kupata ufafanuzi wa fedha shilingi 50,322,585.25 zilizoidhinishwa kama zimetumika katika ujenzi wa mabanda mawili ya mfano, Ofisi ya mtoza ushuru wa

.................................... ....................................

**KATIBU** **MWENYEKITI**

Halmashauri, Ofisi ya Polisi na Vyoo peke yake.

Katibu alijibu kuwa fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya shughuli hizo tu hususani baada ya uamuzi wa kujenga choo chenye matundu 4.

**d)** Mjumbe alitaka kufahamu kama kiasi cha shilingi 200,000/= kitatosha kwa ajili ya kuanzisha shamba moja la mfano la maharage ya soya kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha maharage katika Kata ya Bosha na Mhinduro ifikapo Juni, 2022.

Katibu alijibu kuwa Mashamba wataandaa Wakulima na fedha ni kwa ajili ya kununua mbegu.

**e)** Mjumbe alishauri kuwa ni vizuri yafanyike makadirio ya pamoja kati ya wataalamu na wakulima kujua gharama na ni vizuri shamba darasa limilikiwe na Halmashauri au kama ni kikundi maandalizi yafanyike na Halmashauri na kusimamiwa na Afisa Ugani wa Kata husika.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**MUHT.NA.121/11/2021/2022:TAARIFA YA UKAGUZI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU JANUARI-MACHI 2022.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya Ukaguzi kwa Kipindi cha Robo ya tatu Januari- Machi 2022. ambapo Hoja ziliwasilishwa na kujadiliwa.

**Hoja Na. 5.1 Kutokujaza kitabu cha kutunza kumbukumbu za Manunuzi (Stoo leja).**

Katika ukaguzi wa Mradi wa ujenzi wa Hospitail ya Wilaya ilibainika kuwa vifaa vya ujenzi vinapofika eneo la kazi haviandikwi kwenye stoo leja. Hivyo kutokuwepo kwa mtiririko maalumu wa kubaini vifaa vilivyotumika na ambavyo havijatumika badala yake vifaa vinarekodiwa kwenye leja kuu iliyopo Makao makuu. Mapungufu hayo pia yamejitokeza katika ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 na Miradi mingine ya Halmashuari iliyokaguliwa. Hii ni kinyume na sheria ya fedha ya serikali za mitaa namba 54 (3). LGFM 2009

................................................ KATIBU

................................................ MWENYEKITI

**Maoni ya kamati ya Fedha.** Wajumbe walikubaliana na maoni ya kamati ya ukaguzi

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**MUHT.NA.122/11/2021/2022: MAPENDEKEZO YA KUFUTA HOJA ZA MIAKA YA NYUMA ZA MKAGUZI WA NJE KUANZIA 2010/2011 HADI 2018/2019 KWA MUJIBU WA WARAKA NA. 1 WA WAZIRI MKUU WA MWAKA 2015.**

Katibu aliwasilisha Mapendekezo ya Kufuta Hoja za Miaka ya Nyuma za Mkaguzi wa Nje Kuanzia 2010/2011 Hadi 2018/2019 kwa Mujibu wa Waraka Na. 1 wa Waziri Mkuu wa Mwaka 2015.

Hoja zilizowasilishwa zilikuwa 30 ambapo baada ya majadiliano Wajumbe kwa ujumla walikubaliana kuwa hoja za miaka ya nyuma za mkaguzi wa Nje Kuanzia 2010/2011 Hadi 2018/2019 kwa Mujibu Wa Waraka Na. 1 Wa Waziri Mkuu Wa Mwaka 2015 zifutwe

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe waliipokea na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao hicho.

**MUHT.NA.123/11/2021/2022: TAARIFA YA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI YA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mikopo ya asilimia kumi ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kueleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia Mwezi Machi Halmashauri imeshatoa mikopo kiasi cha Shilingi **185,214,770.00** kwa vikundi 23 ikiwa vikundi **16** ni vya wanawake,**6** vya vijana na kimoja (1) cha watu wenye ulemavu.

Katibu aliiomba Kamati iridhie kukopeshwa vikundi **9** vyenye thamani ya Shilingi **115,140,000.00** ikiwa **4** ni vya wanawake na **5** vya vijana ambavyo tayari vimetembelewa, vimejadiliwa na kupitishwa kwenye kikao cha kamati ya huduma za mikopo cha tarehe 08/04/2022.

Kwa sasa kiasi kilichopo kwenye Akaunti ya wanawake vijana na watu wenye ulemavu ni

.................................... KATIBU

.................................... MWENYEKITI

kutoka Serikali kuu. Mradi huu umeingiziwa kiasi cha Shilingi 150,000,000.00 kwa ajili ya gharama za vifaa na ufundi.

Kazi ambazo zimetekelezwa hadi sasa ni kusafisha eneo ambalo lilikuwa msitu, ujenzi wa msingi, ujenzi wa boma na hatua inayofuata ni ya upauaji.

**CHANGAMOTO**

Moja ya changamoto ya mradi ni Banda la kulala fundi pamoja na vibarua wake halifai kwa kuwa limeezekwa kwa nailoni ambayo kwa sasa imechanika chanika. Kamati iliagiza uongozi suala hili lifanyiwe utaratibu ili wajenzi waweze kupata sehemu ya kulala.

Aidha suala la kuchelewa kwa vifaa ambalo kwa sasa halipo limekemewa kutojirudia ili fundi amalize kazi yake kwa wakati.

**2. UJENZI WA NYUMBA TATU KWA MOJA YA WATUMISHI KATIKA ZAHANATI YA MAZOLA KILIFI**

Mradi huu wa ujenzi wa nyumba 3 kwa 1 ya watumishi katika Zahati ya Kijiji cha Mazola umefadhiliwa na serikali kuu kupitia fedha za UVIKO 19 ambapo kiasi cha shilingi 90,000,000.00 zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Aidha hadi sasa kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na kusafisha eneo kwa nguvu za wananchi, ujenzi wa msingi, ujenzi wa boma, upauaji, upigaji lipu, uwekaji wa njia za mfumo wa umeme, uwekaji wa dari, uwekaji wa fremu za milango na magrili ya madirisha na kusikimu jengo lote.

**MAMBO YALIYOBAINIKA**

Nguvu za wananchi katika mradi kutothaminishwa hata kwa uchache wake. Hata hivyo kulikuwa na mkanganyiko wa maelezo ya wananchi waliojitokeza kuchangia nguvu kazi, ambapo baadhi ya wadau walidai wananchi walijitokeza kuchangia nguvu na Mtendaji pamoja na kamati ya ujenzi walidai watu walioonekana wakifanya kazi katika eneo la ujenzi ni vibarua walioajiriwa na fundi Mkuu.

Hali kadhalika kamati ilielekeza fundi akamilishe kazi zake zilizobaki kabla ya muda wake kukamilika. Hata hivyo kuna kasoro ndogo ndogo nazo zilielekezwa zirekebishwe.

................................ ................................

KATIBU MWENYEKITI

**BARABARA YA KICHANGANI**

Katika mradi huu, kazi ya kupasua barabara ya kichangani hadi Mwanyumba yenye urefu wa km.9 imekamilika na kazi inayofuata ni kutengeneza mitaro, kuweka moramu katika maeneo korofi pamoja na makalavati. Aidha katika hatua nyingine wananchi wa Kata ya Gombero walishukuru sana kwani barabara hiyo imekuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya eneo hilo. Kadhalika wananchi walipongeza sana Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa kuwatembelea.

4. **UJENZI WA VYUMBA VINNE VYA MADARASA SHULE SHIKIZI YA KUZE KIBAGO**

Katika mradi huu ujenzi umetekelezwa kupitia fedha za Mradi wa TCRP ambapo shule hii iliingiziwa kiasi cha Shilingi 80,000,0000.00 kwa ajili ya kujenga vyumba vinne vya madarasa. Katika kutekeleza mradi huo wananchi walifanikiwa kujenga vyumba vinne vya madarasa na ofisi mbili za walimu pamoja na madawati katika vyumba vyote vya madarasa.

**CHANGAMOTO**

Katika kutekeleza mradi kulitokea kuwa na deni ambalo bado wananchi zaidi ya 100 wanadai fedha kwa ajili ya kugonga kokoto kiasi cha shilingi 1,400,000.00 ambapo suala hili linashughulikiwa kiofisi na fedha hizi zitalipwa kwa utaratibu ambao utawekwa na ofisi ili kuondoa kero kwa wananchi na kuwapa haki yao.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa choo katika shule hii ambayo kwa sasa ina wanafunzi 118 ambao wanasoma bila ya choo. Hata hivyo kiasi cha 3,000,000.00 kimeingizwa kwa ajili ya ujenzi wa choo kutoka katika Mfuko wa Jimbo.

Aidha, baadhi ya sakafu zimeanza kuweka nyufa, kamati iliagiza marekebisho yafanyike.

5. **UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU SHULE YA MSINGI NG'OMBENI**

Utekelezaji wa ujenzi wa nyumba hii yenye uwezo wa kubeba familia mbili umekamilika kwa asilimia 90. Mradi huu unatekelezwa kupitia mapato ya ndani ya Halamashauri, ambapo hadi sasa kiasi cha Shilingi 57,000,000.00 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi huu.

Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni kama ifuatavyo: - ujenzi wa msingi, ujenzi wa boma, kupaua, kuweka milango, magrili na kazi za umaliziaji zinaendelea.

..................................
**KATIBU**

..................................
**MWENYEKITI**

**MUHT.NA.131/11/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa kuweza kuchangia hoja zilizowasilishwa kwa kina kwa ajili ya ufanisi katika kuendesha Halmashauri na aliwatakia wajumbe sikukuu njema za kitaifa ambazo ni maadhimisho ya siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na Eid-El-Fitri; alifunga kikao rasmi saa 11:35 Jioni.

**UMETHIBITISHWA NA:**

| | |
|---|---|
| ...................................... | ...................................... |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| ZAHARA MSANGI | AMANI J. KASINYA |
| **JINA** | **JINA** |

**TAREHE** 1/6/2022